WENGINE WAKILALA, KWA WENGINE...

KUMEKUCHA!

JUZUU 2 TOLEO 5

SEPTEMBA 28, 2011

MWAMKO MPYA WA KIFIKRA

MIAKA 50 YA UHURU

CCM, CUF NA CHADEMA

NANI ATASHINDA KWA HOJA AU KWA TUHUMA?



Mgombea wa Ubunge kwa kupitia CDM huko Igunga Mwl. Kashindye (mrefu) akiongozana na viongozi wa Kitaifa wa chama chake Bw. Mbowe na Bw. Slaa

Na Mwandishi Wetu

CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO (CDM) kinaonekana kuwa ni mzigo mkubwa kwa Chama cha Mapinduzi huko Igunga kiasi kwamba madai mbalimbali yanayoelekezwa dhidi yake kuanza kuonekana ni ya vichekesho na kejeli. Tuhuma mbalimbali ambazo zimekuwa zikielekezwa na kuhusishwa na CDM huko Igunga zimeanza kuvuka mipaka na kuanza kuonekana kama baadhi ya mbinu chafu za uchaguzi.

Hata hivyo CCM nayo inaonekana kuwa ni tishio kwa matamanio ya CDM **(inaendelea Uk. 2)**

FIKRA PEVU

JAMII FORUMS
WHERE WE DARE TO TALK OPENLY

TANGAZA HAPA



CCTI
CONSORTIUM OF CONCERNED TANZANIANS INTERNATIONAL
Protecting Our Future · Today

MANJI AWA ADUI WA UHURU WA HABARI TZ?



Na. Mahmoud Rashid

Endapo mahakama zitaendelea kukubali maombi ya mfanyabiashara maarufu nchini Bw. Yusuph Manji ya kutaka kuzuia habari zake kuandikwa au kuonekana kwenye vyombo vya habari kadha wa kadha nchini basi zitakuwa zinashiriki kwa makusudi katika mashambulizi ya wazi, dhahiri na ya makusudi dhidi ya uhuru wa habari nchini.

Bw. Manji ametajwa tangu mwaka 2006 kuwa anahusika moja kwa moja na mojawapo ya wizi wa mabilioni ya shilingi za Kitanzania kutoka benki kuu kwenye akaunti ya masalio ya madeni ya nje maarufu kama EPA. Kwa kupitia kampuni ya Kagoda Agricultural Limited Bw. Manji (Pichani) na kampuni zake kadhaa amejikuta akitajwa tajwa na kuhusishwa na wizi huo na wiki chache tu zilizopita yeye mwenyewe alikiri kuwa ni kweli alinufaika na fedha hizo za wizi – japo alidai kuwa alizirudisha baada ya kubanwa na serikali.Baada ya kashfa ya EPA kuibuliwa mwishoni mwa mwaka 2005 na hasa baada ya kelele za wanaharakati **(inaendelea Uk.)**



M. M. Mwanakijiji

Mhariri

CUF, CCM NA CHADEMA—NANI ATASHINDA KWA HOJA?

(Inatoka Uk. 1) ambapo chama hicho kikongwe kikitumia nguvu zake zote kuhakikisha kuwa jimbo la Igunga haliangukii mikononi mwa upinzani. Hivyo, wana mikakati wake kama wale wa CDM wanashambulia kotekote katika kukionesha kuwa CDM ni chama cha vurugu na udini. Vyama hivyo vimebanana katika kushindana nani kati yao anaweza kuja na tuhuma za kutisha zaidi.

Kumwagiwa tindikali

Tuhuma za kwanza kali ambazo CDM ilihusishwa nazo ni tukio la kijana mmoja ambaye anadaiwa kuwa ni mwana CCM kumwagiwa kile kinachodhaniwa kuwa ni tindikali ambayo ilimuunguza vibaya usoni na baadhi ya sehemu za mwili. Kijana huyo Musa Tesha (24) inadaiwa alimwagiwa tindikali hiyo akiwa katika juhudi za kubandika mabango ya mgombea wa CCM. Mara moja madai yakaanza kutolewa kuwa *wahusika* wa tukio hilo ni CDM.

Hata hivyo madai hayo yalipuuzwa na uongozi wa CDM huku kukiwepo tuhuma kuwa watu waliofanya vitendo hivyo hawahusiani hata kidogo na CDM na hadi hivi sasa hakuna mtu aliyekamatwa kwa tukio hilo licha ya kwamba baadhi ya viongozi wa CCM walidai kuwa Tesha aliwataja kwa majina wahusika wa tukio hilo.

CDM kupeleka "maghaidi" Igunga

Gazeti la Chama cha Mapinduzi la Uhuru likiandika kwenye kurasa zake Septemba 14 lilikuja na madai mazito ambayo yamerudiwa tena na Katibu Mkuu wa Chama hicho kuwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo kimepeleka kundi la maghaidi huko Igunga ili kuharibu kura. "kuna kikundi cha kigaidi kimepelekwa Igunga na CHADEMA, kwa lengo la kuwatisha wanawake na wazee wasijitokeze kupiga kura. Pamoja na kutumia kikundi cha kigaidi ambacho kina vijana 800, CHADEMA pia imeandaa mkakati wa kutengeneza shahada bandia za kupigia kura mkoani Arusha ili zitumiwe na kikundi hicho na vijana wengine wa kihuni. Kwa sasa kikundi hicho kinamwinda mbunge wa Iramba Magharibi, Mwigulu Nchemba, ambaye pia ni Mratibu wa Kampeni za CCM mjini hapa, ili amwagiwe tindikali kama alivyofanyiwa kada wa CCM, Mussa Tesha (24)." Liliandika gazeti hilo.

Hata hivyo madai hayo ambayo ni mazito yanadhalilisha zaidi vyombo vya usalama nchini ambavyo vyote vinasimamiwa na serikali ya Chama cha Mapinduzi. Madai ya kuwa kuna watu wamepata mafunzo ya kighaidi uko Afghanistan au Libya na wakaweza kuingizwa nchini bila kukamatwa (japo wanajulikana) yanatishia zaidi usalama na yanaweza kutumiwa kuonesha jinsi serikali ilivyo dhaifu. Baadhi ya watu walioandika kwenye mitandao mbalimbali wameshangazwa na madai hayo kwani yanadhihirisha kuwa vyombo vyetu vya usalama (polisi, usalama wa taifa, jeshi n.k) ni legelege na dhaifu.

Mmoja wa wachangiaji kwenye mtandao wa JamiiForums ameandika kuwa "Haya ya kutishia watu kwa mgongo wa CHADEMA mara makomandoo,mara magaidi hayana tofauti kubwa na zile propaganda za mwaka jana za Shimbo!.Na inasadikika vile vitisho ni moja ya sababu ya watu wachache kujitokeza kupiga kura,kwa hiyo CHADEMA inabidi wajitahidi kuwapiga dozi ya kudumu(elimu),ili hawa jamaa wasiweze kuwayumbisha wana Igunga katika maamuzi yao,maana CCM wamekata tamaa,wako desparate kuja na upuuzi wowote katika kipindi kilichobaki-Akili zao ziko likizo"

Kubakwa kwa binti ya Kada wa CCM

Mara baada ya tukio la kumwagiwa tindikali tukio jingine likatokea Igunga ambalo nalo kwa sababu zisizoeleweka likahusishwa na CDM badala ya kuchukuliwa kama tukio la kihalifu. Gazeti la Mwananchi liliripoti kuwa "Kada wa CCM, Francisco Msalika amejeruhiwa kwa panga kichwani na binti yake kubakwa baada ya kuvamiwa nyumbani kwake Mtaa wa Benki ya zamani mjini Igunga na watu ambao walimtaka atoe pesa za kampeni. Akizungumza akiwa kitandani katika wodi ya majeruhi katika hospitali hiyo, kada huyo alisema tukio hilo lilitokea juzi kuamkia jana majira ya saa nane za usiku. Alisema alisikia kishindo ambacho kiliuvunja mlango wake wa chumbani na kisha watu hao kummulika kwa tochi kali usoni."

KARIBU JAMIIFORUMS.COM

Hata hivyo tukio hilo linaendelea kuchunguzwa na Jeshi la Polisi. Baadhi ya wanasiasa walianza kulitumia tukio hilo na kuanza kuwaita CDM "wabakaji" kwani binti ya kada huyo ilidaiwa kuwa amebakwa katika tukio la uvamizi huo.

Tukio la kuchomwa banda la kuku

Lakini tukio jingine ambalo limeacha vinywa vya watu wazi ni lile la kuungua kwa banda la kuku la Katibu wa CCM Kata ya Nyandekwa huko Igunga. Tukio hilo lilitokea mwanzoni mwa wiki hii ambapo inadaiwa watu wasiojulikana walitia kibiriti banda hilo la kuku na taarifa hiyo kuripotiwa na gazeti la Mwananchi la Jumatano. Gazeti hilo liliandika kuwa "MATUKIO ya hujuma yanazidi kulitikisa Jimbo la Igunga safari hii watu wasiojulikana wamechoma moto nyumba ya Katibu wa CCM, Kata ya Nyandekwa usiku wa kuamkia juzi.Tukio hilo linahusishwa na wafuasi wa Chadema kutokana na ujumbe wa maandishi uliokutwa umechomekwa katika nyumba hiyo ukisomeka: "Chadema sisi ni wajanja".Katibu huyo, Hamis Makala alimweleza Katibu Mkuu wa CCM, Wilson Mukama aliyemtembelea jana kumpa pole kuwa, kwa muda mrefu amekuwa akiwindwa na wafuasi hao wa Chadema."

Na kuongeza kuwa "Alidai kuwa sababu ya kuwindwa na wafuasi hao inatokana na kukasirishwa na kampeni anazozifanya katika kata hiyo zinazoifanya CCM ikubalike kwa wananchi na kukiacha Chadema kikikosa watu kinapokwenda kufanya mikutano ya hadhara. Nyumba iliyoteketezwa kwa moto ilikuwa ikitumiwa na katibu huyo kwa shughuli za jiko na kuhifadhia kuku." Kada huyo wa CCM alielezea kuwa "Niliposhtuka na kutoka nje nilikuta moto mkubwa unawaka nikapiga yowe kuomba msaada. Lakini majirani walishindwa kuuzima kwa kuwa ulikuwa umesambaa... kuku 15 kati ya 21 waliokuwamo ndani wamekufa"

Baada ya moto kuzimika kwa mujibu wa gazeti hilo Katibu huyo alirudi kwenda kulala na kesho yake alipoamka ndio walikuta hiyo karatasi inayodai kuwa imesema "Chadema sisi wajanja". Hata hivyo imeshindwa kuelekeweka karatasi hiyo iliwezaje kunusurika moto huo au upepo hadi kesho yake asubuhi ambapo ilikuwa ikingojea kuchukuliwa kama ushahidi.Lakini cha **(Inaendelea Uk. 3)**

CCM NA CDM WABANANA

(Inatoka Uk. 2) kushangaza zaidi ni kuwa baadhi ya viongozi wa CCM akiwemo Katibu Mkuu Bw. Wilson Mukama walijitokeza tena kutoa pole na kuilaumu Chadema kwa tukio hilo. Gazeti la Mwananchi limeripoti kuwa bw. Mukama amelaani tukio hiyo kwa kusema kuwa "Ni lazima lilaaniwe kwa sababu halitoi taswira na maana halisi ya kuwa na vyama vingi ambavyo vinapaswa kushindana kwa ubora na sera... hatushindani kwa vitisho, uhuni na hata kumwagiana tindikali"

Hata hivyo kwa mara nyingine tena CDM imelazimika kukana kuhusika na tukio hilo. Kiongozi wa Kampeni ya CDM huko Igunga Bw. Benson Kijaila amepuuzia matukio hayo akisema kuwa "Matukio haya wanayapanga wao wenyewe halafu wanasingizia vijana wetu... kama ni kuchoma hiyo nyumba wameichoma wenyewe ni mpango wao huo"



Mgombea wa Ubunge kwa tiketi ya CCM huko Igunga Bw. Dalaly Kafumu akiombewa kura na Katibu Mkuu wa CCM Bw. Wilson Mukama kijiji cha Itumba, Igunga.

Chadema nayo yaituhumu CCM

Pamoja na kuwa CCM imekuwa ikituhumu CDM kwa kuleta vurugu huko Igunga au kujihusisha na matukio ya kihalifu CDM haijawa pembeni katika kurusha tuhuma mbalimbali dhidi ya CCM ikiwemo madai ya kuandaliwa kwa kundi la vijana katika kile ambacho kinadaiwa kuwa ni "kambi za kighaidi". Madai hayo yametolewa na kurushwa na mtandao wa TV wa CHADEMA ambao unamwonyesha mmoja wa vijana ambao wanadaiwa kupatiwa mafunzo mbalimbali ya kuvuruga uchaguzi.

Pia CDM ilituhumu CCM kuwa iliingiza vijana zaidi ya 20 kutoka Tarime kwa ajili ya kuwatisha watu mbalimbali kupiga kura.

Ni wazi kuwa kwa kadiri kampeni ya uchaguzi Igunga inavyoendelea ndivyo tuhuma mbalimbali ambazo zina lengo la kusababisha hofu ya kisaikolojia kwa wapiga kura zitazidi kutolewa. Watu wengi wameanza kuhusisha kampeni hii ya hofu na vitisho na mbinu ambazo zilitumika wakati wa uchaguzi mkuu mwaka jana ambapo kauli mbalimbali za umwagikaji damu, na vurugu zilitumiwa kuwatisha watu kujitokeza kupiga kura.

Ni wazi kuwa matokeo ya uchaguzi ya Igunga yatategemea sana ni nani anaaminika katika hizi tuhuma mbalimbali na ni kwa kiasi gani uzito wa tuhuma hizi umeathiri fikra za wapiga kura. Kama watu wengi watahofia kujitokeza kupiga kura siku ya uchaguzi kwa sababu ya "hofu" ni wazi kwamba wale watakaojitokeza watakuwa wale ambao wanajisikia salama, ni wanaume na vijana kuliko wanawake **(Inaendelea Uk. 5)**

MANJI AWA ADUI WA UHURU WA UHURU WA HABARI?

(Kutoka Uk. 1) kikosi kazi kiliundwa kwa ajili ya kufuatilia undani wa kashfa hiyo. Kabla kikosi hicho hakijakamiliza kazi yake Gavana wa Benki Kuu Bw. Daudi Ballali- shahidi muhimu wa wizi wa EPA akatoroshwa nchini. Huku nyuma badala ya kuachilia kutumika kwa mfumo wa upepelezi wa makosa ya jinai ukachaguliwa mfumo wa kisiasa ambao ulikuwa nje ya taratibu za uchunguzi wa uhalifu nchini yaani kutumia kikosi kazi ambacho kiliundwa na Ikulu badala ya DPP. Kuundwa kwa kikosi kazi hicho kulisababisha baadhi ya watu kuhoji uwezo wake kisheria kuweza kusaka wahalifu. Hata hivyo hakukuwa na mapingamizi yoyote na wasomi na taasisi mbalimbali ziliridhika na mfumo huo. Kati ya majukumu yake mbalimbali kikosi hicho ilikuwa ni kuhakikisha kuwa fedha zote zilizoibwa toka akaunti hiyo ya EPA ambazo zilizidi dola milioni 133 zinarudishwa mara moja na wahusika wake wote kufikishwa mahakamani.

Hata hivyo tume iliyoundwa haikufata mara moja mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) ambaye aliyatoa katika ripoti yake ya uchunguzi wa akaunti za Benki Kuu kufuatia wizi huo wa EPA. Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya CAG ambayo ilizingatia yaliyokutwa na kampuni ya ukaguzi ya Ernst and Young mambo kadhaa yalitakiwa kufanyika.

Kipengele 4.1 cha ripoti hiyo ya "SIRI" ambayo FikraPevu inayo nakala yake kinasema kuwa CAG amependekeza kwamba "The government should institute a formal criminal investigation by competent law enforcing agencies against the 13 assignee companies and (their) directors, and the officials of BoT involved in the fraudulent payments amounting to TZS 90,359,078,804.13 whose results should form the basis of further action"

Zaidi ya yote yote kipengele kinachofuatia kinasema kuwa "The government should consider initiating legal procedures aiming at recovery of the funds paid to the 13 companies that undeservedly received a total of TZS 90,359,078,804.13. Initially, this can take a form of temporary bank accounts and assets freeze process pending the completion **(Inaendelea Uk. 5)**

Soma bure

NGUVU YA HOJA: MISINGI YA TAIFA LETU NI NINI?

Na. **M. M. Mwanakijiji**

WIKI iliyopita nilianzisha mjadala wa kuhoji kama watu wanafahamu Tanzania kama taifa limejengwa katika msingi gani. Sehemu ya swali hilo lilikuwa kwenye tovuti dada ya Jamiiforums linasema hivi: Kila taifa lina misingi yake.

Misingi ambayo husimama kama maono ya aina ya taifa gani watu wanalitaka kujenga na wananchi wake hujitahidi kuifikia hiyo. Kwa mfano Wamarekani wanachukulia Tangazo la Uhuru na kauli za waasisi wao kuweza kuona misingi yao. Mambo kama Uhuru (liberty) na haki za mtu (individual rights) ni misingi ya Wamarekani.

Je Tanzania ina misingi gani? Je unaifahamu? Je unafahamu Kanuni Nne za mahusiano ya Tanzania? Je unajua ilimaanisha nini kusema wewe ni Mtanganyika au Mtanzania (baada ya Muungano? Je umewahi kujifunza misingi hiyo ukiwa shuleni au chuoni?

Yafuatayo basi ni baadhi ya majibu ya wanachama mbalimbali ambayo waliyachangia katika kuelezea kile ambacho wanaamini ndio msingi wa Taifa letu. Tunapozungumzia msingi tunazungumzia kanuni ambazo kwazo taifa letu limesimama na ya kwamba kanuni hizo zinapovunjwa, kusahaulishwa, au kudharauliwa basi kunadhoofisha ujensi wa taifa letu na maisha ya wale wote wakaao ndani yake.

Nyumba inaweza kujengwa ikapendeza, ikawa na mapambo ya kila aina na hata ikasifiwa kwa jinsi inavyovutia lakini endapo misingi yake haiko imara basi nyumba hiyo ni rahisi kuangushwa au kutikiswa. Misingi inapotikiswa hukimbilii kuziba paa! Misingi ikibomoka watu hawakimbilii kupaka rangi nyumba.

Misingi ya taifa letu basi ni ipi? (tulikaribisha lugha zote mbili)

Let me bet: - Before Arusha declaration I think our moral was laid on

Work and Self-reliance: That our development will depend on our own resources!



Equality: Only on that basis we can work cooperatively

Freedom: Freedom to all; because the individual is not served by the society unless it is his society.

Unity: Unified society where members live and work cooperatively in peace, security and wellbeing- **Arafat**

Mimi nadhani kama taifa, tulikuwa hatuna misingi, ila tu tumekuwa na misingi ya kiitikadi na kichama zaidi na imekuwaikibadilika siku hadi siku, ndiyo maana watanzania wengi hatujui maana ya Uzalendo au utaifa wetu kama watanzania. Hakuna anayeweza kusisimama kutoka chama chochote kile, Dini yoyote ile au Kabila lolote lile akaonyesha uzalendo wa Mtanzania ni upi.

Tofauti na wenzetu wa Taifa kama Marekani, popote utakapo kutana na mmarekani, cha kwanza ni kuuonyesha uzalendo kuwa yeye ni Mmarekani bila kujali antoka ktk kabila, Dini au chama gani. Kwa hiyo Mzee Mwanakijiji, mimi nadhani Msingi mkuu ulikuwa ni ule Uzalendo kuwa Mtanzania, ambao kwa kweli hatukukua nao na wala hata sasa haupo- **We Know Next**

Nimeipenda hii, ngoja niijibu kwa aliyoyapigania Nyerere ambayo yote yalikuwa chini ya kivuli cha utu wa mwanadamu bila kujali rangi, kabila, kipara, wala kibiyongo.

1. Umoja wa Tanzania, umoja wa africa na ikiwezekana kuwe na umoja dunia nzima

2. Na ili kuwe na umoja inabidi tuwe na Amani na utulivu. Hapa Tanzania hilo

lililetwa na Azimio la Arusha - kuleta matumaini kwa wanyonge, na kuweza kuishi na mabepari kwa amani na utulivu

3. Kuondoa manyanyaso, kuondoa ukoloni wa zamani na mamboleo: Makaburi yetu bado yako kule kwa kina Muthalika

4. Kutofungamana na upande wowote wakati wa vita baridi: Hili lilitusaidia sana kuavoid what the guy called automatic conflicts, kwamba wewe ukishakuwa mjamaa, basi 'automatically' unakosana na Mmarekani. Kibiblia sisi tulikuwa 'vuguvugu' katika siasa za dunia, na tuliweza kuchota misaada kutoka Marekani, China, Cuba, Urusi, n.k – **Mzee Madoshi**

Mkuu nadhani we have a problem katika taifa letu kwa kutofahamu misingi ya utaifa wetu lakinni kwa Marekani and especially for the highlighted kumbuka ni vitabu vingi mno, documentaries na movies nyingi mno zimetungwa kuyaelezea hayo. Wagombea uongozi karibu wote wakati wa kampeni huwa wana- go around those words kila wakati, as such si kwa wamarekani tu hata scholars from outside the US wanayafahamu maneno hayo.

With us kikubwa nachokiona ni kupuuzia kila jambo, we don't have a realistic vision. Tumeipuuzia past yetu na that's why in just 50 years tayari kuna watu wameanza kupindisha historia ya taifa hili kwa nguvu kabisa. Ukichukua mawaziri wote na (**Inaendelea Uk. 5)**

HOJA AU TUHUMA?

(Inatoka Uk. 3) wengi na wazee. Vyama vya siasa Igunga na hasa CCM na CDM vinakabiliwa na jaribio kubwa la kuweza kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

Hata hivyo jukumu hilo inaonekana ni gumu sana kwani karibu vyombo vyote vya usalama vimekaa katika hali ya kusubiri matukio yatokee ili waanze uchunguzi na uwezo wao wa kuzuia matukio kabla hayajatokea unaonekana ni mdogo na hivyo vyombo hivyo kwa namna moja kuonekana ni sehemu ya tatizo la usalama huko Igunga.

Ni wazi kwamba kama vyombo vya inteligensia na usimamizi wa sheria vitashindwa kuzuia matukio kabla ya kutokea basi matukio ya uhalifu kwa jina la "kampeni za uchaguzi" yataendelea kutokea na hivyo kuharibu kabisa maana ya dhana ya chaguzi "huru na ya haki"

Masaa machache yajayo yataamua.

MWISHO

MANJI

(Toka Uk. 3) of formal criminal investigation process by competent law enforcing organs." Baadhi ya wahusika wa wizi huu wa EPA tayari wamefikishwa mahakamani isipokuwa wale wa Kagoda Agriculture Limited ambao serikali ilidai kuwa hawajulikani. Kwa muda mrefu tetesi zimekuwepo nchini zikiwahusisha aliyekuwa Mbunge wa Igunga Bw. Rostam Aziz (CCM) na Bw. Yusuph Manji kuwa ndio wahusika wakuu wa kampuni ya Kagoda.

Kwa muda mrefu majina ya Manji na Rostam (pichani) yalihusishwa na kampuni hii hasa kutokana na wao wenyewe au makampuni yao kuonekana kwa namna moja au nyingine kuwa ndio walinufaika na fedha za Kagoda. Lakini zaidi kuhusishwa kwao kumekuja baada ya baadhi ya wadau wakubwa wa harakati za mabadiliko nchini kuweka hadharani kile kinachodaiwa kuwa ni ushahidi "usio na shaka" wa kuhusika kwa wafanyabiashara hawa wawili rafiki na wizi wa EPA na zaidi kushindwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Eliezer Feleshi kuanzisha uchunguzi wake au kuleta mashtaka dhidi yao katika kipindi chote tangu kashfa ya EPA ianze.

Wakati DPP Feleshi akijiweka kando na kusubiri maelekezo "kutoka juu" na kusahau wajibu wake aliopewa kwa mujibu wa Katiba na Sheria Bw. Manji ameamua kuanzisha mashambulizi ya wazi, dhahiri na ya makusudi dhidi ya uhuru wa habari nchini. Mashambulizi hayo kwa kiasi fulani yamefanikiwa kuvitisha vyombo vya habari nchini kuandika habari zozote kuhusu Manji vikihofia kuonekana vinakiuka "amri halali" ya mahakama.

Kijarida chako ukipendacho cha Kumekucha kitakuletea kwa kina sakata la Manji kutumia mahakama kujaribu kuminya uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa Watanzania kupata na kujadili habari kwani mambo ambayo anayadai mahakama iamuru (na baadhi ya mahakama za chini zimekubali) yanatishia haki na uhuru siyo tu wa kuzungumza bali pia yakikubalika bila kukosolewa yatatishia uhuru wa kifikra.

MISINGI YA TAIFA LETU NI IPI?

(Inatoka Uk. 4) wabunge pia raisi ukawaweka kwenye ukumbi na kuwapa 30 minutes watoe jibu la swali lako usijeshangaa kwa nini tuko hapa tulipo! – **Nyambala**

Katika muktadha wa hoja yako, inaelekea misingi ya taifa unayoizungumzia ni ile inayofahamika kwa wengi katika lugha ya Kingereza kama values (au maadili). Mataifa ambayo yameendelea, yamefanya hivyo kwa kuwa yamejengwa kwenye misingi ya kudumu; misingi ambayo huwa ni injini ya ustawi wa jamii na maendeleo ya raia wa taifa hilo kwa ujumla. Ili umelithibitisha kwa kuvitaja vipengele vya misingi ya taifa la Kimarekani na Magna Carta ya Uingereza.

Mifano hii miwili, inaonyesha azma ya jamii ya kisiasa kutaka kuikumbatia demokrasia, siyo tu kama mfumo wa serikali, bali pia kama njia pekee inayomhakikishia 'mtu uhuru wa kutoa fikra na mawazo yake bila kuingiliwa; kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa au mawazo, kupitia chombo chochote cha habari na bila ya kujali mipaka (kifungu cha 19, Tamko la Haki za Binadamu-Universal Declaration of Human Rights)'- **Ludovick Mwijage**

Hivi leo baada ya miaka 50 ya Uhuru, we still watumwa kifikra, kuna watu

wanataka sana tuamini kwamba wakati wa mkoloni babu zetu waliteseka sana, walinyanyaswa na kadhalika lakini ukweli ni kwamba tumebadilisha vichwa vya watawala. Leo hii hatuna viongozi kama tulivyodhamiria na ndio maana bado tunatumia neno WATAWALA WETU. Twende mbele turudi nyuma utaona ya kwamba hao babu na baba zetu ingawa hawakuwa na elimu ya kushika madaraka ya juu wote waliweza kujenga nyumba zao na kufikia Uhuru aghalab kuikuta familia haina hata nyumba. Hadi tunapata Uhuru ilikuwa vigumu sana kuona homeless na binafsi ktk maisha ya ujana wangu sikumbuki kuona homeless, sikumbuki lakini leo hii mkuu Mwanakijiji kama ulivyosema hapo juu ukienda Igunga na vijijini utashindwa kuamini kama hizi ni sehemu za nchi yetu huru. Tushukuru Mungu Mitumba imeficha aibu kubwa sana! – **Mkandara**

Utanzania sio kuzaliwa tu Tanzania ..Ni uwezo wa Kuutafsri Utu kwa Matendo, Fikra na kauli na hilo linapofanikiwa tunampata MZALENDO. NI UTU kutafsiriwa kwenye nyanja zote za jamii ..Utu kwenye Elimu, Utu Kwenye Kilimo, UTU kwenye Ulinzi, UTU katika kugawana Rasilimali za TAIFA, UTU kwenye UONGOZI, UTU kwenye KATIBA, UTU kwenye Muungano, UTU kwenye SIASA za ndani na nje, UTU kwenye AFYA(mtu ni afya), UTU kweneye maendeleo na ujenzi wa UCHUMI, UTU kutafsitriwa kwa kila mwanachi, familia, jamii na hatimaye kuupata UTU WA TAIFA. - **Azimio Jipya**.

Kijiji cha Mwashiku, Igunga. Picha na Victor Makinda



Wiki ijayo tutaliangalia suala hili la Utu kama ahadi ya pekee ya Tanzania kwa wananchi wake. Tutaonesha kuwa Mtanzania ni mtu ambaye anapigania utu wa mwanadamu bila kujali tofauti za dini, rangi, kabila, jinsia au hadhi.


PICHA YA WIKI

RAGE NA MGUU WA KUKU



Kada wa CCM Aden Rage (MB) akiwa na silaha kibindoni. Amedai kuwa hakujua kuwa ana silaha kiunoni!

KATUNI YA WIKI



Unaweza kuunga mkono JamiiForums.com na "Kumekucha". Wasiliana na:

Support@jamiiforums.com au

Kwa PayPal
Mwanakijjji@klhnews.com

Donate now with..


PayPal

KUHUSU 'KUMEKUCHA'

Kijarida cha Kumekucha hutolewa mara kwa mara bure kwa kushirikiana na mtandao wa Jamiiforums.com. Unaweza kuweka matangazo yako kuwafikia wasomaji waliotawanyika sehemu zote nchini, tuandikie support@jamiiforums.com kuuliza jinsi ya kuweka matangazo hapa.

Kuanzia wiki ijayo pamoja na habari za matukio mbalimbali "Kumekucha" itakuletea makala fupi za hoja kutoka kwa waandishi, wanasiasa na wanaharakati mbalimbali. Ili makala yako ifikiriwe kutoka kwenye kijarida chako kipya ukipendacho, tuandikie "mwanakijjji@jamiiforums.com". Makala yake iwe katika lugha ya kiswahili au Kiingereza na ISIZIDI ukurasa mmoja.

MAKTABA YA MIAKA 50 YA UHURU



Baba wa Taifa akiwachekesha kina Askofu Mkuu Desmond Tutu, Katibu wa Madola wa zamani Shridath Ramphal na Askofu Trevor Huddleston—1993

KUMEKUCHA

Mchapishaji

B. G. M Production

Timu ya Waandishi

M. M. Mwanakijjji — Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,

maoni, habari, na ushauri

Kanusho: Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki. Habari zote ni kwa ajiili ya burudani na kuelimishana. Jithibitishie kila usomalo.